

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU**

**SERIKALI KUWAITA KAZINI WATUMISHI WA KADA ZA AFYA**

**Dodoma, Jumatatu 05 Julai, 2021**

Mtakumbuka kwamba tarehe **12 Mei, 2021** Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilitoa taarifa kwa umma ya kupata kibali cha ajira mbadala za kada mbalimbali za afya kutoka Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi na Utawala bora. **Nafasi hizi za ajira na mgawanyo wa kada mbalimbali zilizotokana na watumishi kukoma utumishi wao kwa sababu mbalimbali kama vile kuacha kazi, kufariki na kustaafu.** Nafasi hizo **473** zilitangazwa kwenye Tovuti ya Wizara **ajira.moh.go.tz** kuanzia tarehe **12 Mei, 2021** na kufungwa tarehe **25 Mei, 2021**. Jumla ya maombi yaliyopokelewa kwenye mfumo yalikuwa **19,757** na kati ya hayo waombaji **4,760** hawakukamilisha ujazaji wa fomu hadi hatua ya mwisho. Hivyo, maombi yaliyofanyiwa uchambuzi ni **14,997**.

Baada ya uchambuzi kufanyika jumla ya maombi **9,338** yalikitidhi vigezo vya **kuajiriwa kutokana na tangazo letu**. Aidha, ili kuwapata waombaji wa kujaza nafasi zinazohitajika vigezo vya ziada vifuatavyo vilitumika.

- i. Waombaji wenye ulemavu.
- ii. Waombaji waliohitimu elimu ya mwaka 2018 na kurudi nyuma.
- iii. Waombaji wenye ajira za mikataba ya muda.
- iv. Waombaji wenye umri chini ya miaka 45.

Baada ya uchambuzi zaidi kufanyika jumla ya waombaji **473** waliohitajika wamechaguliwa. Watumishi hawa wamepangwa maeneo yenye uhitaji na upungufu mkubwa wa watumishi.

**Waombaji waliokosa sifa wametokana na sababu zifuatazo;**

- i. Hawakukamilisha ujazaji wa fomu hadi hatua ya mwisho
- ii. Kukosa sifa za kimuundo za kada husika.
- iii. Kutoambatisha vyeti muhimu wakati wa kuomba ajira.
- iv. Kutokuwa na Leseni za kitaaluma ikiwa ni pamoja na Leseni kuisha muda wake.
- v. Baadhi ya waombaji kuomba kazi katika kada ambayo sio ya taaluma yake.

**Mgawanyiko wa nafasi hizi 473 kwa kada mbalimbali kulingana** na jinsi ambayo tulipokea kutoka Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi na Utawala bora, **umeanishwa kwenye Jedwali hapa chini;**

<b>NA</b>	<b>KADA</b>	<b>IDADI YA NAFASI ZILIZOIDHINISHWA KWENYE KIBALI</b>	<b>IDADI YA WALIOCHAGULIWA</b>
1	DAKTARI BINGWA	8	8
2	DAKTARI DARAJA II	23	23
3	DAKTARI (MENO)	5	5
4	AFISA MUUGUZI	17	17
5	AFISA MUUGUZI MSAIDIZI	67	67
6	MUUGUZI	139	139
7	AFISA AFYA MAZINGIRA	3	3
8	AFISA AFYA MAZINGIRA MSAIDIZI	3	3
9	FIZIOTHERAPIA	2	2
10	FUNDI SANIFU VIFAA TIBA	1	1

11	KATIBU WA AFYA	1	1
12	FAMASIA	7	7
13	MTEKNOLOJIA( MENO)	3	3
14	MTEKNOLOJIA( MIONZI)	5	5
15	MTEKNOLOJIA( MAABARA)	10	10
16	MTEKNOLOJIA( MACHO)	5	5
17	MTEKNOLOJIA MAS Aidizi (MAABARA)	8	8
18	MS Aidizi WA AFYA	166	166
		<b>473</b>	<b>473</b>

Naomba nitumie fursa hii kuwasihwa waombaji wa kazi za ajira zinazotangazwa kuwa makini wakati wanapowasilisha maombi ya kazi. Aidha, waombaji wanaosimamiwa na Mabaraza mbalimbali ya Kitaaluma wahakikishe wanakuwa na Leseni hai za kufanyia kazi.

Waombaji wote waliofaulu na ambao majina yao yameorodheshwa kwenye tangazo hili wanatakiwa kuripoti Ofisi za Wizara ya Afya zilizopo katika Ukumbi wa Chuo cha Uuguzi na Ukunga Mirembe kuanzia tarehe **05 - 09 Julai, 2021**. Aidha, wanatakiwa kufika na vyeti halisi vya elimu na taaluma yake alivyotumia kuomba ajira ikiwa ni pamoja na nakala mbili (2) ya;

- i. Nakala ya cheti cha kuzaliwa;
- ii. Wasifu binafsi (CV)
- iii. Nakala ya Kitambulisho/namba ya Uraia (NIDA); na
- iv. Nakala ya vyeti vya elimu ya Sekondari (Kidato cha Nne na Sita);
- v. Nakala ya vyeti vya taaluma;
- vi. Nakala ya Cheti cha Mafunzo kwa Vitendo (Internship);
- vii. Nakala ya Cheti cha usajili kutoka Baraza husika (Valid Licence);

- viii. Nakala ya Ithibati ya vyeti vya elimu na taaluma (Accreditation na Equivalence) kutoka TCU na NECTA kwa wale waliosoma vyuo nje ya nchi pamoja na wale waliosoma Sekondari nje ya nchi/Mitaala ya nje;
- ix. Iwapo majina yako yanatofautiana katika vyeti vyako pamoja na cheti cha kuzaliwa hakikisha unawasilisha kiapo cha majina (Deed Pool) kutoka kwa Msajili wa Viapo na Kusajiliwa na Msajili wa Hati, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi;
- x. Picha mbili (2) Passport Size.

Mtumishi atakayeripoti na 'Transcript' tu au kuwa na nakala pungufu ya vielelezo tajwa juu hatapokelewa.

Waombaji wote ambao majina yao hayakuonekana katika tangazo hili wafahamu kuwa hawakupata nafasi, hivyo wasisite kuomba tena wakati nafasi za kazi zitakapotangazwa.

**Imetolewa na**



Prof. Abel N. Makubi

**KATIBU MKUU (AFYA)**